

KANISA ANGLIKANA TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

ASKOFU MAIMBO WILLIAM FABIAN MNDOLWA ATAWAZWA KUWA ASKOFU MKUU WA SABA WA KANISA ANGLIKANA TANZANIA.

Askofu Maimbo William Fabian Mndolwa, Askofu wa Dayosisi ya Tanga ametawazwa kuwa Askofu Mkuu wa Saba wa Kanisa Anglikana Tanzania leo tarehe 20 Mei, 2018 katika siku ya Bwana ya Pentekoste. Askofu Mndolwa ametawazwa rasmi katika ibada iliyofanyika kwenye Kanisa Kuu la Roho Mtakatifu la jijini Dodoma. Ibada ya kutawazwa kwa Askofu Mndolwa, iliongozwa na Askofu wa Sita wa Kanisa hili Dkt. Jacob Erasto Chimeledya na imehudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali na Madhehebu ya Dini kutoka ndani na Nje ya Tanzania. Ibada hiyo ilihudhuriwa pia na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, ambaye alimwakilisha mgeni rasmi, Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Ibada hiyo ilikuwa na wageni mbalimbali toka nje ya nchi, akiwemo Askofu wa Dayosisi ya Rochester ya Uingereza, **Right Reverend James Langstaff**, ambaye alimwakilisha Askofu Mkuu wa Canterbury, **The Most Revd and Rt Hon Justin Welby**. Wageni walioshiriki ibada hiyo, waliguswa zaidi na hotuba ya amani iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu Majaliwa Kassim Majaliwa ambaye alitumia vifungu mbalimbali vya Biblia kuwataka Wakristo wote na Waumini wa Madhehebu mbalimbali nchini kuulinda na kuithamini amani iliyopo sasa. Mhe. Waziri Mkuu aliwahimiza waumini kufanya kazi na kuzingatia misingi ya dini ambayo ni amani, upendo na mshikamano utakaoleta maendeleo kwa Taifa.

Katika hotuba yake, Askofu Mkuu Mndolwa aliahidi kuendeleza amani ya nchi kwa kushirikiana na Serikali. Amesema, alipoongea na Mhe. Rais kabla ya ibada, alimweleza nia yake ya kutembelea Ikulu na kukutana na Rais wa Zanzibar ili kuendeleza jitihada za kudumisha amani na kuleta maendeleo. Pia Askofu Mkuu Mndolwa alisisitiza kuwa atahakikisha anakutana na viongozi wa madhahebu yote ya dini kwa lengo la kujadiliana kuhusu suala la amani ya Taifa.

Naye Waziri Mkuu akitoa hotuba yake, alisisitiza kuwa Kanisa Anglikana Tanzania limekuwa mstari wa mbele katika kusimamia amani na kwamba ataendelea kushirikiana na Kanisa kwenye mambo yote ya msingi kwa manufaa ya Taifa. Kipekee amemshukuru Askofu Mkuu anayemaliza muda wake, Askofu Mkuu Dkt. Jacob Chimeledya kwa kusimamia vyema misingi ya Kanisa Anglikana katika kipindi chake chote. Mhe. Waziri Mkuu aliisifu kazi iliyofanywa na Maaskofu wote wakuu waliotangulia. Alimpa nasaha

Askofu Mkuu Maimbo kwamba asiogope kwani kiatu walichovaa watangulizi wake, kinamtosha. Mhe. Waziri Mkuu aliahidi kuwa Serikali itashirikiana kwa karibu na Askofu Mkuu Mndolwa katika kuwaletea waumini wa Anglikana maendeleo .

Kwa mujibu wa Katiba ya Kanisa Anglikana Tanzania ya mwaka 1970, Askofu Mkuu Mndolwa ataongoza Kanisa kwa kipindi cha miaka mitano.

Kanisa linawaomba waumini wote kumwomba Askofu Mkuu Maimbo katika utumishi wake.

Askofu Mkuu Mndolwa alizaliwa Korogwe-Tanga, Tanzania, mnamo tarehe 24 Novemba, 1969. Wazazi wake ni Mndolwa Fabian Maimbo na Kauye-Agnes Mbelwa. Askofu Mndolwa ni Askofu wa Kanisa Anglikana Dayosisi ya Tanga. Aliingia katika daraja takatifu la Askofu Tarehe 04 Septemba, 2012. Askofu Mkuu Mndolwa ni Mwanahistoria ya Kanisa na ana Shahada ya Uzamivu katika masuala ya Theolojia, Kanisa na Siasa. Askofu Mkuu Mndolwa ameo. Mke wake ni Chenga Frida ambaye wamebarikiwa kupata watoto wanne: Msagati-Katindi, Prisna-Kauye, Tahona na Challenge.

Kwa neema ya Mungu taarifa hii imetolewa kwa umma na:

Rev Can Dr Mecka Ogunde

Katibu Mkuu,

Kanisa Anglikana Tanzania

20 Mei 2018

ANGLICAN CHURCH OF TANZANIA



PRESS RELEASE

BISHOP MAIMBO WILLIAM FABIAN MNDOLWA HAS BEEN ENTHRONED AS THE SEVENTH PRIMATE AND ARCHBISHOP OF THE ANGLICAN CHURCH OF TANZANIA.

Today, May, 20,2018 in the day of Pentecost, the Anglican Church of Tanzania has enthroned Bishop Maimbo William Fabian Mndolwa, the bishop of the Diocese of Tanga, as the seventh Primate and Archbishop of the Anglican Church of Tanzania. Bishop Mndolwa has been officially enthroned in the service held at the Cathedral of the Holy Spirit in city of Dodoma. The enthronement service which was officiated by Archbishop Dr. Jacob Erasto Chimeledya, was attended by various religious leaders and government officials, including the Prime Minister of the United Republic of Tanzania, Honorable Majaliwa Kassim Majaliwa, who represented the guest of honour, President of the United Republic of Tanzania, Honourable Dr. John Pombe Joseph Magufuli.

The service was attended by various international guests, including the bishop of Rochester, UK, **Right Reverend James Langstaff**, who represented the Archbishop of Canterbury, **The Most Revd and Rt Hon Justin Welby**. Many visitors were impressed by the symbols of peace in Tanzania by witnessing the presence of senior government officials from non-Christian denominations using the Bible to convey a message of peace to the community.

In his sermon, Archbishop Mndolwa promised to promote peace in the country in cooperation with the government. He said, when he spoke to the President, he registered his intention to call on the State House and meet with the President of Zanzibar to promote peace and prosperity. Archbishop Mndolwa also insisted that he will meet with other Christian and non-Christian leaders for the sake of maintaining national peace.

As the Prime Minister delivered his speech, he emphasized that the Anglican Church of Tanzania has been in the forefront of promoting peace and that he will continue to cooperate with the church in all aspects of significant importance for the nation. He personally expressed his gratitude to the former Archbishop, The Most Rev Dr. Jacob Chimeledya for his outstanding achievements. Also, the Prime Minister praised the work done by the former Archbishop's predecessors. He advised the newly enthroned Archbishop that he should not fear as the shoes worn by his predecessors, completely fit him. The Prime Minister said he will closely cooperate with the newly enthroned Archbishop and assured him that he will identify him with favorite form of naming: Maimbo William Fabian Mndolwa.

Under the Constitution of the Anglican Church of Tanzania, Bishop Mndolwa will serve as Archbishop for a period of five years.

The church invites all Christians to pray for the Primate and Archbishop Mndolwa in his service.

Archbishop Mndolwa was born in Korogwe-Tanga, Tanzania, on 24/11/1969. His parents are Mndolwa Fabian Maimbo and Kauye-Agnes Mbelwa. Archbishop Mndolwa is the bishop of the Anglican Diocese of Tanga. He was consecrated into the order of a bishop on 04/9/2012. Archbishop Mndolwa is a Church historian, he has a PhD degree in theology, Church and Politics. Archbishop Mndolwa is married. His wife is Chenga Frida whom together they have been blessed with four children: Msagati-Katindi, Prisma-Kauye, Tahona and Challenge.

By God's grace this statement has been issued to the public by:

Rev Can Dr Mecka Ogunde
The Secretary General,
The Anglican Church of Tanzania
20 May, 2018